



Taarifa ya Maamuzi ya Kamati ya Sera ya Fedha

Kamati ya Sera ya Fedha (Monetary Policy Committee) ya Benki Kuu ya Tanzania ilifanya mkutano wake wa kawaida tarehe 5 Oktoba 2020, ili kutathmini hali ya sasa ya mwenendo wa uchumi na mwelekeo wake. Kamati ya Sera ya Fedha imeridhika kuwa uchumi unaendelea kuimarika licha ya athari za janga la ugonjwa wa virusi vya Corona (COVID-19). Kwa kuzingatia viashiria mbalimbali, uchumi unatarajiwa kukua kwa asilimia 5.5 mwaka 2020.

Kamati ya Sera ya Fedha imeridhika na mwenendo wa viashiria mbalimbali vya uchumi mpana ambavyo vimeendelea kuwa imara na kubakia ndani ya malengo yaliyokubalika kikanda. Kasi ya mfumuko wa bei imeendelea kuwa katika kiwango cha tarakimu moja cha wastani wa asilimia 3.3 kwa mwezi Julai hadi Agosti 2020. Matarajio ni kuwa mfumuko wa bei utaendelea kubakia kati ya asilimia 3 hadi 5 mwaka 2020/21, kama ilivyokadiriwa awali. Matarajio haya yanatokana na mwenendo mzuri wa uzalishaji na ugavi wa mazao ya chakula kwa kiwango cha kutosha nchini, utulivu wa thamani ya shilingi dhidi ya fedha za kigeni, wastani wa bei ya mafuta kuendelea kubakia katika viwango vya chini, pamoja na sera madhubuti za fedha na kibajeti. Aidha, akiba ya fedha za kigeni imeendelea kubakia katika viwango vya juu, zaidi ya dola za Marekani bilioni 5, kiasi ambacho kinatosheleza uagizaji bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa takribani miezi 6. Nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje imeendelea kupungua kufuatia kuongezeka kwa mauzo nje ya nchi, hususan dhahabu na korosho. Hali hii imechangia kwenye utulivu wa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya sarafu nyingine kubwa duniani.

Vilevile, kutokana na utekelezaji na usimamizi thabiti wa sera ya fedha, hali ya ukwasi katika uchumi imeendelea kutosheleza mahitaji mbalimbali ya shughuli za kiuchumi na kusababisha kupungua kwa viwango vya riba za mabanki. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi umeendelea kwa kasi ya kuridhisha licha ya changamoto mbalimbali zitokanazo na janga la ugonjwa wa COVID-19 kwenye mnyororo wa usambazaji bidhaa na huduma katika soko la dunia. Mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa asilimia 6.8 kwa mwaka ulioishia mwezi Agosti 2020, ukiwa ni juu ya ukuaji wa asilimia 5.5 uliofikiwa mwezi Juni na Julai 2020. Kamati ya Sera ya Fedha inatarajia kwamba ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi utaendelea kuimarika na kufikia lengo la asilimia 11.6 mwaka 2020/21. Makadirio haya yatachangiwa zaidi na sera nzuri ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi katika kukuza uchumi, pamoja na kuendelea kufunguka kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi. Sekta ya

benki imeendelea kuwa imara na salama ikiwa na ukwasi na mitaji ya kutosha kusaidia shughuli za kiuchumi.

Kamati ya Sera ya Fedha imeridhika pia na mwenendo wa sekta ya nje ambayo imeendelea kuimarika kufuatia kufunguka kwa baadhi ya shughuli za kiuchumi katika soko la dunia baada ya athari za janga la ugonjwa wa COVID-19 kupungua kiasi. Aidha, katika nusu ya kwanza ya mwaka 2020 ukuaji wa uchumi wa dunia umepungua, hali inayotokana kwa kiasi kikubwa na kusimamishwa kwa shughuli nyingi za kiuchumi katika mataifa yaliyoendelea kufuatia hatua zilizochukuliwa katika kudhibiti kuenea kwa ugonjwa wa COVID-19. Ukuaji wa uchumi wa dunia unatarajiwa kutengamaa katika siku zijazo kufuatia kuendelea kufunguka kwa shughuli za kiuchumi katika nchi nyingi duniani.

Kamati ya Sera ya Fedha iliridhika na utekelezaji imara wa sera ya kibajeti ambayo imeendelea kusimamiwa kwa dhati kwa kuzingatia misingi ya kiuchumi. Matumizi ya serikali yameendelea kuboreshwa na kusimamiwa kwa umakini mkubwa kwa kuzingatia uwepo wa tija na utekelezaji wa miradi ya maendeleo, sambamba na maboresho ya ukusanyaji mapato ya serikali ambayo yameendelea kuimarika.

Kutokana na mwenendo mzima wa uchumi mpana, na matarajio ya kuendelea kwa utulivu wa mfumuko wa bei katika viwango vya chini, Kamati ya Sera ya Fedha imeiagiza Benki Kuu ya Tanzania kuendelea kutekeleza sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi kwenye uchumi ili kuchochea zaidi ukuaji wa uchumi na kudumisha utulivu wa sekta ya fedha.

GAVANA
BENKI KUU YA TANZANIA